Hali ya haki za kibinadamu yazidi kuimarika: THBUB

Na Mwandishi Wetu,Singida

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB),Mohamed Khamis Hamad amesema kuwa hali ya haki za binadamu nchini inaendelea kuimarika kutokana na uelewa wa watu juu ya haki za binadamu na utawala bora.

Mohamed alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Salmin Amour iliyopo katika Manispaa ya Singida,ambapo alisema hiyo ni kutokana na watu kuwa na uelewa wa kuibua masuala ya uvunjifu wa haki za binadamu.

"Watu wanaibua masuala mbalimbali yanatokea katika jamii lakini pia Serikali inachukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa haki za watu zinalindwa,"alisema Mohamed.

Aidha,Mohamed aliongeza kuwa THBUB inaendelea na jukumu la kutoa elimu kwa jamii na kufanya uchunguzi kwa lengo la kuzuia vitendo vya kikatili huku akitoa wito kwa Wazazi kukomesha vitendo vya kikatili kwa Watoto.

Naye Mwalimu, Veronica Emmanuel alitoa shukrani kwa THBUB kwa kutembelea na kutoa elimu kwa wanafunzi na Walimu wa Shule hiyo kwani elimu hiyo itawasaidia Wanafunzi na Walimu kujua haki na wajibu wao ili waweze kujisimamia nakufanya maamuzi sahihi hususan pale wanapokutana na vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Kwa upande wake Mwanafunzi wa Kidato cha Tatu,Omar Mwinyi alishukuru pia ujumbe wa THBUB kwatoa elimu hasa ya haki za mtoto ikiwemo haki ya kulindwa.

"Mimi nitakua balozi kwa wanafunzi wenzangu kwakupinga vitendo vya kikatili na kuwaelimisha juu ya haki zao" alisema mwinyi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso akizungumza hivi karibuni wakati wa kikao cha kamati hiyo cha kupokea na kujadili taarifa ya utelekezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kilichofanyika jijini Dodoma. (Na Mpigapicha Wetu)

Askofu Malasusa aanika athari za ndoa za utotoni

Na Judith Ferdinand,Times, Mwanza

MKUU wa Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania(KKKT),Askofu Dkt. Alex Malasusa,amesema ndoa za utotoni zinachangia uwepo wa talaka nyingi nchini.

Kutokanana hali hiyo ametoa wito kwa jamii kuhakikisha suala la ndoa hizo linafikia mwisho kwa ajili ya ustawi wa taifa na watoto hususani wa kike ambao ndio waathirika zaidi.

Askofu Malasusa,alitoa kauli hiyo Januari 20,2025,wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari 31 kutoka mikoa na vyombo mbalimbali nchini,kuhusu ndoa za utotoni,yanayofanyika mkoani Mwanza kwa siku tatu,chini ya mradi wa hapana marefu yasiyokuwa na mwisho, unaotekelezwa na KKKT wenye kauli mbiu isemayo,"Ndoa za utotoni,sasa mwisho".

"Wito wangu kwa jamii ya Watanzania,sasa suala la ndoa za utotoni lifike mwisho kwani zinaondoa upendo,ndio maana tuna tatizo kubwa la talaka nchini.

Kwa sababu mmoja wa wana ndoa hawakua na uamuzi wa kuingia katika ndoa. Sisi viongozi wa dini lazima tuone kama Biblia inavyosema, ndoa na iheshimiwe, sasa watoto wengi wanasukumwa katika ndoa na hawana uhuru wa kuingia katika ndoa,"alisema Askofu Malasusa na kuongeza:

"Sheria zipo lakini kila siku wazazi wanabuni mbinu mpya ikiwemo kuwataka watoto wao wajifelishe ili waende kuwaoza,waandishi wa habari ibueni hayo mambo na ikiwezekana tuleteeni viongozi wa dini,kwamba mzazi fulani amefanya hiki na hiki,na mimi nitakuwa mstari wa mbele,kusimama na kwenda kuwatoa watoto hao, kwani Tanzania tumefanikiwa mambo mengi na hili waandishi wa habari mkilichukulia kwa nguvu tutafanikiwa,".

Askofu Malasusa,alisema pia ndoa za utotoni zinapoteza uelekeo wa mtoto wa kike huku akitolea mfano mtoto aliyeokolewa kwenye ndoa za utotoni wilayani Kwimba mkoani Mwanza, ambaye ameendelea na masomo ya Uhandisi wa Meli "Marine Engineering",ambapo kama kungekuwa hakuna watu wa kumuokoa taifa lingempoteza Mhandisi wa baadae.

"Watoto waendelee kufundishwa juu ya haki zao ili waweze kujitetea wenyewe na kujisimamia na kujua kuwa wanamaisha zaidi kuliko kukimbilia kwenye ndoa.

Ni jambo la aibu mtoto kuolewa katika umri mdogo ambapo wazazi hasa wa kiume wanaona watoto wa kike kama rasilimali za kiuchumi na kupigia hesabu ana watoto wangapi ambao wataolewa ili pate mahari,".

Msimamizi Mkuu,program ya maisha endelevu na uwezeshaji KKKT,Patricia Mwaikenda,alisema maisha ya ndoa za utotoni yamekuwa safari ndefu katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania.

Ambapo safari hiyo imeanzia tangu kwa mabibi,mama,dada,rika moja,watoto na wajukuu ambao wamekuwa wakiozeshwa.

Hivyo kanisa likaona sasa suala la ndoa za utotoni lifike mwisho linalochangiwa na mila na desturi kandamizi, kwa kuanzisha mradi ambao utafanya viongozi wa dini kuwa mstari wa mbele kukataa jambo hilo,kutoa elimu kwa watoto wa kike na kiume kuweza kukata na kupinga suala la ndoa za utotoni,watoto wa kike kuweza kujitete.

"Tangu mradi huo uanze mwaka juzi, kanisa limeisha okoa watoto watatu ambao walikuwa wanaozeshwa kwa nguvu kutoka Wilaya ya Kwimba binti alikuwa amemaliza kidato cha nne matokeo yametoka akawa anaozeshwa,Mchungaji akapiga simu akashirikiana na Serikali ukawekwa mtego,mhusika akakamatwa siku ya kulipa mahari,huyu binti sasa anasoma marine engineering,fikiri kichwa kizuri hivyo kinapelekwa kupika ugali kwa kupelekwa kwenye ndoa hata hawezi,".

Mkurugenzi Mtendaji wa Upendo Media, Neng'ida Johhannes, alisema kama kanisa wananjivunia kuwa sehemu ya mapambano dhidi ya ndoa za utotoni,kwani wasichana wanaoolewa katika umri mdogo wanapoteza fursa ya kupata elimu huku afya zao zinakuwa hatarishi pamoja na kuingia kwenye ndoa ambazo hazina upendo wala heshima.

"Ndoa za utotoni ni tatizo ambalo linakabili pia nchi yetu,na nchi nyingi zinazoendelea kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanya hapa nchini na za kimataifa,zinaonesha Tanzania mikoa ambayo inaongoza kuwa na kiwango cha juu cha ndoa za utotoni ni Shinyanga,Tabora,Mara,Dodoma na Lindi, huku chanzo kikitajwa kuwa ni umasikini na mila kandamizi,"amesema Johhannes.

Hata hivyo,aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha inakuwa mstari wa mbele kuhimiza jamii iweze kuachana na mila kandamizi na ukawaida unasababisha ndoa za utotoni.

Akiwasilisha mada katika mafunzo hayo,Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Mwanza,Baraka Makona,alisema,ndoa za utotoni zinafanyika zaidi katika maeneo ya vijijini katika jamii maskini na katika mikoa ya Magharibi,Kusini na Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania.

Ambapo wanawake wanne kati ya kumi sawa na asilimia 37 wenye umri wa miaka 15-49 wanaoish vijijini waliolewa wakiwa watoto ikilinganishwa na wanawake wawili kati ya kumi sawa na asilimia 21 wanaoishi mijini.

Kwa mujibu wa taarifa za UNICEF, zinaonesha asilimia 21 ya wanawake vijana huolewa kabla ya kufikia umri wa miaka 18,hii inamaana kuwa wanawake milioni 650 wanaolewa chini ya umri unaotakiwa sawa na wanawake milioni 12 kila mwaka.

Huku idadi kubwa ya ndoa za utotoni asilimia 37 zinatokea Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo na Tanzania ikiwemo.